Jina: …….. Nambari yako: ……...

Sahihi ya mtahiniwa……...

Tarehe: ……..

102/3
KISWAHILI
Karatasi ya 3
FASIHI
Machi/Aprili 2011
Muda : Saa 1 ¾

MTIHANI WA MWIGO WA PAMOJA WA MOKASA

Hati ya Kuhitimu Kisomo cha Sekondari – Kenya
102/3
KISWAHILI
Karatasi ya 3
FASIHI
Machi/Aprili 2011
Muda : Saa 1 ¾

Maagizo

(a) *Jibu maswali manne pekee*
(b) *Swali la kwanza ni la lizima*
(c) *Maswali hayo mengine matatu yachaguliwe kutoka sehemu zilizobaki yaani kifo kisimani, Tamthilia, Ushairi na Fasihi simulizi*
(d) *Usijibu maswali mawili kutoka sehemu moja*
(e) *Karatasi hii ina kurasa 5 zilizopigwa chapa*
(f) *Watahiniwa ni lazima wahakikisha kwamba kurasa zote za karatasi hii zimepigwa chapa sawasawa na kuwa maswali yote yamo.*

© 2011, Kamati ya MOKASA

HADITHI FUPI

K.W WAMITILA: *Mayai Waziri wa Maradhi na Hadithi Nyingine*

1. Lazima

" Karibu ndugu yangu. Waumini ni kukirimiana tunashukuru, alhamdulilahi, sifa zote nzuri zake Maulana tusaidiane kuinusuru dini yake muumba."

(i) Eleza muktadha wa dondoo hili (Alama 4)

(ii) Taja mbinu moja ya sanaa kwenye dondoo hili (Alama 1)

(iii) Jadili hulka zozote nne za mnenewa (Alama 4)

(iv) Kwa kuzingatia hadithi zingine zozote ttatu kitabuni, dhihirisha namna maudhui ya unafiki yanavyokuzwa (Alama 9

(v) Tetea anwani ya hadithi rejelewa (Alama 2)

TAMTHILIA

KITHAKA WA MBERIA: *Kifo Kisimani*

Jibu swali la 2 au la 3

2. (a) "Tayari mateso ndiyo hewa wanayopumua wanabutangi." Thibitisha ukweli wa kauli hii" (Alama 10)

(b) Upofu miongoni mwa baadhi ya wanabutangi ulikwamisha juhudi za ukombozi dhidi ya utawala dhalimu wa mtemi Bokono." Fafanua (Alama 10)

3. "Uovu usio na kifani? Siasa haina uovu usio na kifani kuna mbinu tu. Mbinu za kuwanyamazisha wasioridhika….. usipomnyoosha adui, adui atakunyoosha.

(a) Eleza muktadha wa dondoo hili (Alama 4)

(b) Eleza umuhimu wa mnenaji (Alama 6)

(c) Linganua sifa za mnenaji wa mnenewa (Alama 6)

(d) Jadili maudhui yoyote mawili yanayoendelezwa na mnenaji (Alama 4)

S.A MOHAMED: *Utengano*

Jibu swali la 4 au la 5

4. Anasahau hata kwamba damu ni nzito kuliko maji. Lakini haidhuru

(a) Eleza muktdha wa dondoo hili (Alama 6)

(b) Taja na ufafanue mbinu ya lugha iliyotumiwa katika dondoo hili(Alama 4)

(c) Eleza sifa za anarejelewa katika dondoo hili (Alama 4)

(d) Fafanua maudhui mawili yanadokekwa na dondoo hili (Alama 6)

5. Riwaya ya utengamao inabainisha wazi yanaoikumba jamii. Thibitisha kauli hii kwa kutoa mifano mwafaka (Alama 20)

FASIHI SIMULIZI

6. (a) Jadili vijipera vya maghani kwa kurejelea sifa za kila mojawapo (Alama 5)

(b) Eleza sifa tano za ngomezi katika fasihi simulizi (Alama 5)

(c) Jadili namna tano za uundaji wa misimu katika fasihi simulizi (Alama 5)

(d) Fafanua muundo wa nyimbo (Alama 5)

USHAIRI

7. Soma shairi A na B kisha jibu maswali yanayofuata

SHAIRI A

Nikiwa na njaa na matambara mwilini
nimehudumika kama hayawani
kupigwa na kutukanwa
kimya kama kupita kwa shetani

Nafasi ya kupumzika hakuna
ya kulala hakuna
ya kuwaza hakuna
basi kwani hili kufanyika

Ni kosa gani lilotendeka
Liloniletea adhabu hii isomalizika?
Ewe mwenwe urukae juu mbinguni
Wajua lililomo mwangu moyoni

Niambie pale mipunga inapopea
Ikitema miale ya jua
Mamaangu bado angali amesimama akinisubiri?
Je nadhari yake hijitokeza usoni
Ikielekea huku kizuizini?

Mpenzi mama, nitarudi nyumbani
Nitarudi hata kama ni kifoni
Hata kama maiti yangu imekatikatika
Vipande elfu, elfu kumi
Nitarudi nyumbani
Nikipenya kwenye ukuta huu
Nikipitia mwingine kama shetani,
Nitarudi mpenzi mama……
Hata kama ni kifoni

SHAIRI B
Baada ya dhiki faraja,
Yangu malelengu, masaha yatukutile,
Yatutia na tewengu, kuzipa nyoyo uwele,
Subira ni kilimwengu, mtu kuiweka mbele,
Hakuna tabu milele, baada dhiki faraji.

Loote likikufika, yafaa uzingatile,
Ni amri ya Rabuka, mtenda hili na lile,
Mambo yanavyogeuke, na watu vile vile,
Hakuna tabu milele, baada dhiki faraji.

Leo una kutukuka, kwa utajo wa riale,
Vibindo vimefutuka, mifuko nayo tele,
Mpanda ngazi hushuka, kula bando na mawele,
Hakuna tabu milele, baada dhiki faraji.

Hali iwapo hii, mambo yakuzungukile,
Usiondoe bidii, fanya hima wende mbele,
Kwa mawazo usidhii, kudhana hivi na vile,
Hakuna tabu milele, baada dhiki faraji.

Fanya kwa kudhamiria, tabu ikuepukile,
Utazame kila nia, njema sio upotole,
Penye nia pana njia, ya kufikia vilele,
Hakuna tabu milele, baada dhiki faraji.

Mwenye kujisadia, kutumika jambole,
Mungu humkusadia, msaada wa tendole,
Mwisho akampatia, sitawa huku na kule,
Hakuna tabu milele, baada dhiki faraji.

Basi vikikupotea, ulovitaka vikele,
Usikae na kulia, kutafaruri vya kale,
Karibu ba baidia, vitafute pope pole
Hakuna tabu milele, baada dhiki faraji.

Maswali

(a) Mashairi haya ni ya aina gani? (Alama 2)
(b) Eleza muundo wa ubeti wa 5 wa shairi B (Alama 4)
(c) Linganisha maudhui ya ubeti wa 5 ya shairi A na yale ya ubeti wa 6 ya shairi B (Alama 4)
(d) Andika ubeti wa 3 wa shairi kwa lugha ya nathari (Alama 4)
(e) Eleza uhuru wa ushairi ulivyotumika katika shairi A na shairi B (Alama 4)
(f) Tambua tamathali mbili za lugha zinazojitokeza katika shairi A na Katika shairi B (Alama 2)